







# Orientation to Ontario




1-855-626-0002
https://orientationontario.ca





## EPUKA UTAPELI

### TOVUTI GHUSHI NA UTAPELI WA MTANDAO

Wahalifu wanaweza kunakili tovuti halisi au kujenga inayoonekana kuwa ya kitaalamu. Tovuti zinaweza kudai kuwa tovuti rasmi za Serikali ya Kanada au mmoja wa washirika wao. Wengine wanaweza kudai kutoa mikataba maalum ya uhamiaji au kuhakikishiwa kazi zenye mishahara mikubwa. Wanafanya hivi ili kuiba vitambulisho na kuwalaghai watu ili wawalipe pesa.

- Ikiwa tovuti inadai kutoa ofa maalum kwa watu wanaotaka kuhama, ondoka kwenye tovuti hiyo. Madai haya ni ya uongo.
- Angalia anwani ya URL kwenye upau wa anwani wa kivinjari chako unapotua kwenye tovuti. Inapaswa kuendana na anwani uliyoandika.
- Usiwahi kuweka maelezo ya faragha isipokuwa kuwe na ishara ya kufuli kwenye dirisha la kivinjari au “https://” mwanzoni mwa anwani ya wavuti ili kuonyesha kuwa ni salama.

### UTAPELI WA BARUA PEPE NA WA MAANDISHI

Unaweza kupata barua pepe inayoonekana kana kwamba imetoka kwa shirika halali kama vile taasisi za fedha, biashara au mashirika ya serikali. Inaweza kukuuliza maelezo ya faragha kama vile tarehe yako ya kuzaliwa, manenosiri au maelezo ya kadi ya mkopo. Wakati mwingine barua pepe hiyo itakuambia utembelee tovuti ghushi.

- Mashirika yanayotambulika hayatawahi kukuomba taarifa zako za kibinafsi kupitia barua pepe au maandishi.

- Mashirika yanayotambulika hayatawahi kukuomba taarifa zako za kibinafsi kupitia barua pepe au maandishi.
- Ukipata aina hii ya barua pepe, usibofye viungo vyovyote au kutoa taarifa yoyote kukuhusu.
- Ikiwa una shaka yoyote kuhusu mahali barua pepe ilitoka, hakikisha kuwa umeangalia utambulisho wa mtumaji. Utapeli wa barua pepe kwa kawaida hutumwa kutoka kwa anwani ya faragha au anwani ya barua pepe ya tovuti isiyolipishwa (Yahoo, Hotmail au Gmail) na si kutoka kwa Serikali ya Kanada "gc.ca" au akaunti ya barua pepe ya "canada.ca"
- Puuza na ufute mawasiliano kutoka kwa anwani zisizojulikana na usasishe kingavirusi yako kwenye vifaa vyote.
- Usijibu ujumbe ghushi, hata kujiondoa, na usifungue viambatisho vyovyote au kufuata viungo vyovyote.

### UTAPELI WA SIMU

Wahalifu wanaweza kujaribu kuwahadaa watu kwenye simu kwa kujifanya wanatoka IRCC (Asasi ya Forodha, Wakimbizi na Uraia Kanada), Canadian Revenue Agency (Shirika la Ukusanyaji Ushuru la Kanada) au polisi. Maafisa katika IRCC (Asasi ya Forodha, Wakimbizi na Uraia Kanada), CRA (Shirika la Ukusanyaji Ushuru la Kanada) au polisi hawatakupigia simu kukuuliza kuweka pesa, kuhamisha pesa au kutoa mikataba maalum kwa watu wanaotaka kuhama. Wakati fulani wanaweza kuwasiliana nawe kwa simu ili kupata maelezo zaidi ili kuendelea kushughulikia ombi, au kuuliza hati zaidi.

Funded by / Financé par :

Ontario

Immigration, Refugees and Citizenship Canada

Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

- Watu wanaweza kutumia utapeli wa simu ili kuiba pesa au utambulisho wako.
- Kuwa mwangalifu sana na utapeli wa simu unaoomba maelezo kama vile kadi za mkopo, nambari za akaunti ya benki au maelezo yoyote ya malipo.
- Ukipigiwa simu ya kutiliwa shaka, kata simu mara moja na uwasiliane na polisi wa eneo lako ili kuripoti. Unaweza pia kuwasiliana na Kituo cha Kupambana na Ulaghai cha Kanada.

## MAMBO YA KUKUMBUKA

- Serikali ya Kanada au polisi hawatawahi kutumia lugha ya fujo au ya vitisho.
- Serikali ya Kanada haitawahi kukuuliza malipo ya aina yoyote kwa njia ya simu, barua pepe au ujumbe mfupi wa maandishi.

CRA (Shirika la Ukusanyaji Ushuru la Kanada) haitawahi kukutumia barua pepe au ujumbe mfupi wa maandishi ikiomba pesa au malipo kupitia kadi za mkopo za kulipia kabla, kadi za zawadi au uhamishaji wa kielektroniki wa Interact.

IRCC (Asasi ya Forodha, Wakimbizi na Uraia Kanada) haitawahi kuwasiliana nawe kwa simu, barua pepe au ujumbe mfupi wa maandishi ikiuliza maelezo yako ya kibinafsi. Wakati fulani wanaweza kuwasiliana nawe kwa simu ili kupata maelezo zaidi ili kuendelea kushughulikia ombi, au kuuliza hati zaidi.

Serikali ya Kanada haitumi visa kwa barua pepe.

## CANADIAN ANTI-FRAUD CENTRE (KITUO CHA KUPAMBANA NA ULAGHAI CHA KANADA)

The Canadian Anti-Fraud Centre (Kituo cha Kupambana na Ulaghai cha Kanada) (CAFC) ni shirika kuu nchini Kanada ambalo hukusanya habari na taarifa za uhalifu kuhusu masuala kama vile ulaghai mkubwa wa uuzaji, ulaghai wa ada ya mapema, ulaghai wa mtandao na malalamiko ya wizi wa vitambulisho. Ili kujifunza jinsi ya kujikinga tembelea antifraudcentre.ca

### MAELEZO MUHIMU:

Ripoti ulaghai, wizi na uhalifu mwingine kwa idara ya polisi ya eneo lako.

Sambaza barua pepe zisizotakikana au za kutiliwa shaka kwa Spam Reporting Center (Kituo cha Kuripoti Ulaghai) katika spam@fightspam.gc.ca

### JE, UNAJUA?

Iwe umetapeliwa au kulengwa na tapeli, unapaswa kuripoti kila wakati. Wasiliana na Canadian Anti-Fraud Centre (Kituo cha Kupambana na Ulaghai cha Kanada.) (1-888-495-8501) au Ofisi ya Ushindani (1-800-348-5358) kwa ushauri wa wapi pa kupiga ripoti..

## RASILIMALI:

Canadian Anti-Fraud Centre:
antifraudcentre.ca

Competition Bureau:
competitionbureau.gc.ca

Government of Canada:
canada.ca

The Little Black Book of Scams:
competitionbureau.gc.ca





